**Zeitschrift:** Acta Tropica

**Herausgeber:** Schweizerisches Tropeninstitut (Basel)

**Band:** 44 (1987)

**Heft:** 2: A longitudinal study in a rural Tanzanian community 1982-1984

**Seite**

**Nutzungsbedingungen**

Die ETH-Bibliothek ist die Anbieterin der digitalisierten Zeitschriften. Sie besitzt keine Urheberrechte an den Zeitschriften und ist nicht verantwortlich für deren Inhalte. Die Rechte liegen in der Regel bei den Herausgebern beziehungsweise den externen Rechteinhabern. Siehe Rechtliche Hinweise.

**Conditions d'utilisation**

L'ETH Library est le fournisseur des revues numérisées. Elle ne détient aucun droit d'auteur sur les revues et n'est pas responsable de leur contenu. En règle générale, les droits sont détenus par les éditeurs ou les détenteurs de droits externes. Voir Informations légales.

**Terms of use**

The ETH Library is the provider of the digitised journals. It does not own any copyrights to the journals and is not responsible for their content. The rights usually lie with the publishers or the external rights holders. See Legal notice.

**Download PDF:** 29.04.2025

**ETH-Bibliothek Zürich, E-Periodica, https://www.e-periodica.ch**

zao ya biashara kama nyanya hulimwa pamoja na mahindi ya muda mfupi (chalula). Kilimo ni duni cha kutumia jembe la mkono. Idadi ya watu inazidi kuongezeka kuliko kiasi cha ardhi. Hii inamaanisha ardhi kutumiwa sana na mwisho kuchoka. Uchunguzi umeonyesha kuwa kulima ardhi isiyorutuba kunaathiri mavuno na lishe ya kijiji. Uchunguzi umependekeza kuwepo kwa wahudumu wa kilimo kijijini. Watu hawa-wachaguliwe toka kijiji na wanakijiji. Wapewe mafunzo mafupi na Idara ya kilimo wilayani ili wawe washauri kijijini kuhusu kilimo na kiungo muhimu kati ya kijiji na Bwana/Bibi Shamba wa Kata/Tarafa. Vile vile uchunguzi umeshauri utunzaji wa ardhi na kubadilisha mazao na kuchanganya baadhi ya mazao ambayo yanaweza kurutubisha udongo.

*Huduma za afya ya msingi*

Tathmini iliyofanywa na Taasisi pamoja na Ofisi ya mganga mkuu wa wilaya, imeonyesha kuwa utekelezaji wa mpango huo wa huduma za afya ya msingi ni muhimu. Huduma hizo zinathaminiwa na wanakijiji na kuimarisha ushirikishaji wa wanakijiji katika mpango mzima wa uchunguzi. Wahudumu wa afya walimudu kutoa huduma za kutibu magonjwa madogo madogo ya malaria/homa, kumuwa na kichwa, vidonda, kuumwa na tumbo, kifua na kikohozi. Wagonjwa kati ya 500–600 walihudhuria kila mwezi. Wastani wa wagonjwa 5–10 walipewa vyeti vya rufaa kwenda zahanati ya karibu (km 2–8) na hospitali teule ya wilaya (km 15). Wastani wa mahudhurio ya kila mwanakijiji kwa mwaka ni 10 na wastani wa mahudhurio kwa siku ni 20–30. Mahudhurio makubwa ni ya wagonjwa wa homa/malaria, kuumwa na kichwa.

*Tiba ya magonjwa*

Kila mwaka tangu 1982–1984 baada ya uchunguzi, wananchi kwa kupitia serikali ya kijiji na wahudumu wa afya walipewa majibu ya vipimo. Cheti cha majibu kilionyesha ugonjwa alioonekana nao, wakati na mahali pa kutibiwa. Magonjwa yaliyoonekana wakati wa uchunguzi ni malaria, safura, kichocho, ameba na giardia. Malaria ilichukua asilimia kubwa na hasa kwa watoto kati ya mwezi mmoja na mwaka mmoja. Wananchi wote watoto kwa wakubwa walioonekana na magonjwa hayo walitibiwa. Hata hivyo athari ya matibabu hayo haikuwa kubwa na badala yake jitihada kubwa zilisisitizwa kukinga magonjwa hayo hasa kichocho na safura.

Hayo ni matokeo ya awali ya mradi. Mradi huu ulipangwa kutekelezwa kwa muda wa miaka kadhaa. Matokeo ya uchunguzi tangu 1982–1984 na shughuli mbalimbali katika kutekeleza mradi huo ni za awali. Mradi unaendelea. Mradi wa kusambaza maji safi kijijini umekwisha anza na unaendelea. Mpango wa kuimarisha usafi wa mazingira kwa kuchimba na kujenga vyoo vya kudumu karibuni utaanza. Njia zote hizo za kuinua hali ya afya ya kijiji cha Kikwawila zitazidi kuimarishwa sambamba na utekelezaji wa mpango wa taifa wa huduma za afya ya msingi. Tathmini ya mradi mzima itakuwa inafanywa ilikupata